

## Jitolee Kuomba!

Paulo anamwandikia kiongozi mchanga wa kanisa Timotheo (1 Timotheo 2:1-8) kumwelekeza na kumtia moyo katika huduma kwa kanisa lililo na changamoto nyingi. Paulo anatumia neno “wote” sana, kutukumbusha kuwa tumeitwa kwa ajili ya kuwaomba watu wote kwa sababu Mungu anataka watu wote wakombolewe kwa sababu hata Yesu Kristo alikufa msalabani kwa ajili ya kuwaokoa wanadamu wote.

“Wote” ni kila mmoja; watu wa hadhi ya juu na ya chini, walio na elimu na wasio na elimu; maskini kwa tajiri, wema kwa waovu; wanaodhihaki wengine na wale wanaodhihakiwa. Kwa yeyote yule, maisha yao ya siku za nyuma si hoja kwa sababu Mungu anataka kuwapa mema aliyowawekea. Anawapenda na sisi pia imetupasa kuwapenda pia. Je, kuna jambo linalopendeza zaidi ya kuzama katika maombi na kuwaomba mahitaji yao kwa Mungu?

Mbali na kuomba jamii zetu, Paulo anatuhimiza kuwaomba walio katika uongozi na serikali, hata kama tunatofautiana nao au hawakubaliani nasi. Tukiomba amani na hekima kwa wale walio mamlakani wamfahamu na kumjua Mungu, atakapowabadilisha je, tutaona mabadiliko kiasi gani? Si katika maisha yetu au ya jamii zetu tu, bali katika taifa nzima, bara (Afrika) na ulimwengu wote kwa jumla.

Yesu pia alitufunza kuomba maadui zetu na wale wanaotutesa. Hili ni jambo gumu, ila tunafaa kukumbuka mawaidha ya Paulo kuomba watu “wote.” Mungu anaweza kutusaidia kuwaomba tusioweza kuwaomba. Pia tunaweza kutumia karama zetu kuomba. Kwa mfano tukikosa maneno sahihi ya kuomba tunaweza kuomba kwa ndimi (lugha) au tunaweza kutabirika watu na hali kwa vifungu vya Biblia. Kutembea katika jamii tukiomba kunaweza kuonyesha ushuhuda mkuu kwa wale walio karibu nasi na vile vile kudhihirisha uweza na nguvu za Mungu katika maeneo haya.

Tunataka Mungu atawale na abariki kule kote tutakanyaga katika maeneo haya, pamoja na watu tunaokutana nao. (Joshua 1:8, Kumbukumbu la torati 11:24). Vikundi vya maisha/uzima ni mfano wa kanisa katika jamii linaloanzishwa na watu wanaokusanyika kuomba jamii.

### Zingatia!

Mwezi huu unaweza kuunganisha watu kutoka makanisa na jamii tofauti ili wajumuike pamoja kuomba au kutembea pamoja wakifanya maombi. Ikiwa unajuana na watu kutoka maeneo na jamii tofauti basi kwa nini usiandae msururu wa mikutano ya maombi au matembezi ya maombi.


### Omba:

- 1) Watu wa Mungu watashirikiana kufikia na kuboresha jamii.
- 2) Watu wa Mungu watashirikiana kufikia na kuboresha jamii.
- 3) Omba kwamba mahitaji ya jamii yatatimizwa na pia watu watabadilishwa.



“Shukurani kwa Dignity ninakua kwa neno la Mungu. Watu wametambua jinsi nilivyokua. Jumapili iliyopita, niliahidi kuwa nitaenda kuomba na mtu mmoja. Alikuwa na jinamizi (ndoto mbaya za kutisha). Tangu tulipoomba naye ndoto mbaya zimekwisha na hali imekuwa tulivu.”

**- John, Mwinilunga, Zambia**



Somo hili limewezeshwa na “Kuomba Jamii yangu” somo linalopatikana katika kitabu cha Misingi Toleo la 3 - Maisha Huumba, ambacho unaweza kupata katika tovuti hapa:

**[dignityonline.org.uk/publications](https://dignityonline.org.uk/publications)**